OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

WILAYA YA UKEREWE

HALMASHAURI YA KIJIJI CHA BUZEGWE

MKATABA WA MUDA

MKATABA WA KUPANGISHA ARDHI YA KIJIJI CHA BUZEGWE KWA AJILI YA KUTEKELEZA MRADI WA UFUGAJI WA SAMAKI

[MKATABA NA. LGA/092/2022-2023/N/.01..]

BAINA
YA

HALMASHAURI YA KIJIJI CHA BUZEGWE

NA

M/S MEMBI FISHERIES LIMITED,

UMEANDALIWA NA:-
OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W).
HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE..
1 Br. ya Halmashauri,
33682 Bukongo
S.L.P.41,
Nansio-UKEREWE.
simu:+225 282 515 056/ +225 685 30 4 646
E-mail:ps@ukerewedc.go.tz
Tovuti:www.ukerewedc.go.tz

MEI 2023

MKATABA WA MUDA

_ MKATABA WA KUPANGISHA ARDHI YA KIJIJI CHA BUZEGWE KWA AJILI YA KUTEKELEZA MRADI WA UFUGAJI WA SAMAKI

MKATABA HUU umefungwa leo hii tarehe 15 mwezi Mei mwaka 2023

BAINA YA

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUZEGWE, ambayo ni mamlaka ya Serikali za Mitaa iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 [ikisomwa pamoja na marekebisho yake], yenye makao na anuani yake Halmashauri ya Kijiji cha Buzegwe, 1 Br. ya Halmashauri, 33682 Bukongo, S.L.P. 41, Nansio-**UKEREWE**. (ambayo katika mkataba huu itajulikana kama ``Halmashauri``) ambayo itarithisha wabia, wakala na warithi wake kwa upande mmoja;

NA

MEMBI FISHERIES LIMITED, ambayo ni kampuni halali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 [ikisomwa pamoja na marekebisho yake] yenye makao na anuani yake P.O. Box 546,Geita-TANZANIA(ambayo katika Mkataba huu itajulikana kama ``Kampuni``) ambayo itarithisha wabia, wakala na warithi wake kwa upande mwingine.

UTANGULIZI

(a) KWA KUWA, Halmashauri kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 [ikisomwa na marekebisho yake pamoja na sheria nyingine zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania] ina mamlaka ya kuandaa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji kwa ajili ya kutekeleza mpango wa matumizi bora ya ardhi ya Kijiji iliyo katika mamlaka yake katika nyanja mabalimbali ikiwemo utunzaji wa mazingira katika maeneo ya fukwe za vyanzo vya maji pamoja na kutenga maeneo ya uwekezaji.

(b) KWA KUWA, Halmashauri katika kutekeleza mamlaka yake ya kupanga na kuendeleza ardhi yake inaweza kufanya kazi hiyo yenyewe au kwa kutumia wabia, wakala, watu binafsi, kampuni au taasisi nyingine.

(c) KWA KUWA, Halmashauri imeamua kuendeleza ardhi ya Kijiji kwa kutenga eneo eneo la Ziwa Viktoria pamoja na sehemu ya eneo la ardhi kwa ajili ya kutekeleza mradi wa mradi wa ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika Kitongoji cha irondo Mashariki.

(d) NA KWA KUWA, ili kutimiza adhma tajwa hapo juu, Halmashauri imepokea maombi kutoka kwa kupitia barua yenye Kumbukumbu Namba MEMBI/out-going/002 ya tarehe 25/03/2023 kwa ajili ya kuomba ridhaa ya Serikali na Wananchi wa Kijiji cha Buzegwe kuridhia uwekezaji wa mradi wa ufugaji wa samaki katika Kitingoji tajwa hapo juu kwa njia ya vizimba.

(e)NA KWA KUWA, wanachi wa Kijiji cha Buzegwe kupitia mapendekezo ya Halmashauri na Mkutano Mkuu wa Kijiji kwa hiari yao wenyewe wameridhia na kukubali kuipangisha Kampuni eneo la Halmashauri lilitajwa hapo juu kwa masharti ya mkataba huu.

HIVYO BASI MKATABA HUU UNATHIBITISHA KWAMBA PANDE ZOTE MBILI ZIMEKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:-

IBARA YA KWANZA
MASHARTI YA JUMLA

1.0. NYARAKA ZIFUATAZO ZITASOMWA PAMOJA NA MKATABA HUU

1.1. Barua ya maombi ya kupangishwa eneo la kutekeleza mradi wa kufuga samaki kwa njia ya vizimba ya tarehe 25/03/2023;

1.2. Barua ya Halmashauri ya kukubali maombi ya Kampuni ya tarehe 28/03/2023;

1.3. Mhtasari wa Serikali ya Kijiji cha Buzegwe wa tarehe 27/03/2023;

1.4. Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kijiji cha Buzegwe wa tarehe 09/05/2023;

1.5. Nakala ya nyaraka za Kampuni;

Nyaraka tajwa hapo juu zitasomwa pamoja na kuwa sehemu ya mkataba huu na iwapo utatokea mkanganyiko katika tafsiri,

nyaraka hizo zitatafsiriwa kwa mtiririko kuanzia nyaraka ya kwanza hadi ya mwisho.

IBARA YA PILI
KAZI ZINAZOKUSUDIWA KUTEKELEZWA

2.1. KWAMBA, **Kampuni** itatekeleza kazi za:-

i. ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba;
ii. kuzalisha vifaranga vya samaki;
iii. kuuza chakula cha samaki wa kufugwa;
iv. kuuza samaki wabichi;
v. kutoa ushauri wa kitaalam wa ufugaji wa samaki.

2.2. KWAMBA, Kampuni itafanya kazi tajwa hapo juu kwa gharama zake yenyewe kwa kununua vifaa na kugharamikia mafundi/wataalam husika.

IBARA YA TATU
ENEO LA UTEKELEZAJI WA MRADI

3.1. KWAMBA, Kampuni itatekeleza mradi wa ufugaji wa samaki katika eneo lililopo Nansio Mjini katika Kitongoji tajwa hapo juu kilichopo ndani ya Halmashauri.

IBARA YA NNE
MASHARTI YA UTEKELEZAJI WA MRADI

4.1. KWAMBA, Kampuni itaanza utetekelezaji wa mradi baada ya kuoneshwa na kukabidhiwa eneo la mradi na Halmashauri.

4.2. KWAMBA, Kampuni haitaanza kutekeleza mradi bila kufanya tathmini ya uharibifu wa mazingira pamoja na kupata kibali kutoka Mamlaka ya Udhibiti na Uhifadhi wa Mazingira.

4.3. KWAMBA, iwapo Kampuni itashindwa kuanza kutekeleza mradi ndani ya miezi sita (06 tangu terehe ya kusaini mkataba huu, Kampuni itakuwa imekiuka masharti ya mkataba huu. Kwa hiyo, itanyang`anywa eneo husika na eneo hilo kupewa mwombaji mwingine.

4.4. KWAMBA, bila kuathiri msharti ya aya ya 4.3. ya kipengere hiki, iwapo kampuni itashindwa kutekeleza masharti ya mkataba huu, kazi zilizokwishaanza kutekelezwa zitafanyiwa tathmini ya gharama zilizotumia na kurejeshewa gharama hizo kwa Kampuni na mwombaji mwingine.

4.5. KWAMBA, wakati wa utekelezaji wa mradi mtaalam wa Halmashauri au mtaalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe atakuwa na haki ya

kuingia katika eneo la mradi muda wowote wa kazi kwa ajili ya kukagua ujenzi unavyoendela na kutoa maelekezo.

IBARA YA TANO
DHAMANA YA MKATABA

5.1. KWAMBA, kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi Kampuni itailipa Halmashauri pesa taslimu kiasi cha shilingi milioni sita (Tzs. Tzs 6,000,000/=) ambazo ni sawa na malipo ya awali ya pango kwa kipindi cha **mwaka mmoja (01)** ikiwa ni dhamana au uthibitisho wa nia ya kukamilisha utekelezaji wa mradi.

5.2. KWAMBA, Iwapo Kampuni itashindwa kukamilisha kutekeleza mradi husika kama iliyoelezwa ndani ya mkataba huu fedha za kodi ya pango zilizolipwa kama dhamana hazitarejeshwa.

5.3. KWAMBA, bila kuathiri masharti mengine ya mkataba huu Kampuni itatakiwa kuwa na leseni ya biashara, Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN),au kitambulisho chochote kinachotambuliwa na Serikali ambapo nakala za vitambulisho hivi vitaambatanishwa kwenye mkataba huu.

IBARA YA SITA
MASHARTI BAADA YA MRADI KUKAMILIKA

6.1. KWAMBA, baada ya mradi kukamilika na kuanza kufanya kazi husika Kampuni itawajibika kulipa kodi ya pango pamoja na tozo zilizowekwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe.

6.2. KWAMBA, Kampuni itawajibika kufanya biashara kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya kufanya biashara ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba kama inavyotolewa mara kwa mara na mamlaka husika.

6.3. KWAMBA, kwa kipindi chote cha uhai wa mkataba huu, Kampuni hairusiwi kumpangisha, kuuza au kumkodisha mtu mwingine, kampuni au taasisi yoyote eneo la mradi au mradi husika bila kupata idhini awali ya maandishi kutoka kwa Halmashauri. Aidha, Kampuni haitakiwi kufanya marekebisho au ukarabati wowote katika eneo la mradi bila kupata idhini awali ya maandishi kutoka kwa Halmashauri.

6.4. KWAMBA, ili kuondoa shaka, Halmashauri haitatambua gharama zozote zilizotumka katika kufanya marekebisho au ukarabati katika eneo la mradi husika ambazo hazijaidhinishwa kwa maandishi na Halmashauri.

JK

6.5. KWAMBA, bila kuathiri masharti mengine ya mkataba huu, Kampuni itawajibika kufanya usafi na kutunza mazingira ya yanayozungulka eneo la mradi kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya usafi na utunzanzaji wa mazingira.

6.6. KWAMBA, Mpangaji atawajibika kuhakikisha kwamba mradi na mali zote zilizomo ndani yake zinakuwa katika hali ya usalama muda wote.

IBARA YA SABA
WAJIBU WA HALMASHAURI

7.1. KWAMBA, Halmashauri kupitia Mhandisi wa Ujenzi au Afisa Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya itasimamia ubora wa utekelezaji wa mradi kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kutoa maelekezo kwa Kampuni katika kila hatua ya utekelezaji.

7.2. KWAMBA, wakati wa utekelezaji wa mradi husika Mhandisi wa Ujenzi au Afisa Uvuvi wa Halmashauri au Mwakilishi wake atakuwa na haki ya kuingia katika eneo la mradi muda wowote wa kazi kwa ajili ya kukagua ujenzi unavyoendela na kutoa maelekezo.

IBARA YA NANE
FIDIA YA HASARA

8.1. KWAMBA, Halmashauri haitalipa fidia au kiasi chochote ambacho Kampuni itawajibika kisheria kulipia kuhusiana na madai yoyote, madhara kwa mtu yeyote au kikundi cha watu au kampuni kutokana na / au kusababishwa na uzembe wa Kmapuni katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba huu.

IBARA YA TISA
ADHA

9.1. KWAMBA, Kampuni haitasababisha au kuruhusu kufanyika kitendo chochote , jambo lolote au kitu chochote ambacho ni adha au kinachoweza kuwa adha wakati wa utekelezaji wa mkataba huu.

IBARA YA KUMI
TAFSIRI

10.1. KWAMBA, lugha rasmi kwa ajili ya majadiliano juu ya mkataba huu itakuwa ni Kiswahili. Aidha, suala lolote au swali litakalohusiana na tafsiri ya maneno/ neno lolote lililotumika katika mkataba huu litatafsiriwa kulingana na maana au jinsi lilivyotumiwa kulingana na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wakati huo.

IBARA YA KUMI NA MOJA
USULUHISHI

11.1. KWAMBA, mgogoro wowote au kutoelewana kunakoweza kutokea au kunakoambatana na au kunakohusiana na utekelezaji wa mkataba huu, utasuruhishwa kwa njia ya majadiliano na ikishindikana mgogoro utatatuliwa kwa njia ya Mahakama.

IBARA YA KUMI NA MBILI
MAREKEBISHO

12.1. KWAMBA, marekebisho, mabadiliko, kupunguzwa au kuongezwa kwa masharti ya mkataba huu vitafanyika wakati wowote iwapo tu kuna maafikiano ya kimaandishi baina ya pande zinazohusika katika mkataba huu.

IBARA YA KUMI NA TATU
MUDA WA MKATABA

13.1. KWAMBA, mkataba huu utatekelezwa kwa kipindi cha **miaka kumi (10)** kuanzia tarehe 15 ya mwezi 05 Mwaka 2023 hadi tarehe 15 ya mwezi 05 Mwaka 2033 vinginevyo uwe umesitishwa kama inavyoelezwa ndani ya mkataba huu. Hata hivyo, mkataba huu utakuwa unafanyiwa marejeo kila baada ya mwaka mmoja(01).

IBARA YA KUMI NA NNE
UMILIKI BAADA YA MKATABA KUFIKIA UKOMO

14.1. KWAMBA, baada ya muda wa mkataba huu kufikia ukomo, Kampuni itawajibika kukabidhi umiliki wa eneo la mradi kwa Halmashauri.

14.2. KWAMBA, ili kuondoa shaka, baada ya muda wa mkataba huu kufikia ukomo Kampuni haitakuwa na mamlaka ya umiliki wa eneo la mradi husika kwa mujibu wa mkataba huu. Kwa hiyo, kama itampendeza kuendelea kutumia eneo la mradi husika kwa shughuli nyingine Kampuni itawajibika kusaini mkataba mwingine kwa mujibu wa mazingira na sheria za kipindi hicho.

IBARA YA KUMI NA TANO
USITISHWAJI MKATABA

15.1. Pande zote mbili zitakuwa na haki ya kusitisha mkataba huu baada ya kutoa notisi ya siku therathini (30) kwa upande mwingine ikieleza sababu za kusitisha mkataba huu.

15.2. Hata hivyo, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kusitisha mkataba huu iwapo:-

(a)Kampuni itashindwa kutekeleza mradi husika ndani ya miezi sita tangu tarehe ya kusaini mpataba huu;

(b)Kampuni itashindwa/itakaidi kulipa kodi ya pango au

(c)iwapo Kampuni itakiuka masharti mengine ya mkataba huu.

15.3. Aidha, Kampuni inaweza kusitisha mkataba huu iwapo:-

(a)itashindwa kutekeleza mradi husika kwa wakati;

(b) iwapo Halmashauri ya Kijiji itakiuka masharti ya mkataba huu.

IBARA YA KUMI NA SITA

MAKUBALIANO NA SHUGHULI ZA ZAMANI

16.1KWAMBA, mkataba huu hautahusisha mkataba wowote wa nyuma (kama upo) na pande zote mbili zimekubaliana kuwa hakuna ujulisho, dhamana, au ahadi yoyote ambayo imetolewa na ambayo haikuingizwa katika mkataba huu.

KWA SHUHUDA, PANDE ZOTE ZIMEWEKA SAINI KWENYE MAKATABA HUU KAMA INAYOONEKANA HAPA CHINI, LEO HII TAREHE. 15 **YA MWEZI** MEI **MWAKA** 2023.

KWA UPANDE WA HALMASHAURI YA KIJIJI CHA BUZEGWE

(1) MWENYEKITI WA HALMASHAURI
JINA: VICENTIUS B. JUSTUS
SAINI: Bmfustus
NAMBA YA SIMU: 0769919099

MWENYEKITI WA SERIKALI YA KIJIJI
BUZEGWE-UKEREWE

muhuri wa moto

(2) MTENDAJI WA KIJIJI
JINA: NDAITI M. WILLIAM
SAINI:
NAMBA YA SIMU: 0745114164

AFISA MTENDAJI
KIJIJI CHA BUZEGWE
UKEREWE

MBELE YA
JINA Kevin K. Rwekiro
SAINI
WADHIFA Msajili

COUNCIL SOLICITOR
UKEREWE DISTRICT COUNCIL
P.O. BOX 41
NANSIO
UKEREWE

Bmfustus

12

KWA UPANDE WA KAMPUNI

1. JINA. HUSSEIN H MALOGI.....
   SAINI. Hmalogi.....
   WADHIFA. AFISA USAFIRISHAJI.....
   NAMABA YA SIMU. 742 733877.....

2. JINA. FRANK F. MACHUMU.....
   SAINI. .....
   WADHIFA. MKURUGENZI - AFISA MTENDAJI MKUU.....
   NAMBA YA SIMU.....

MEMBI FISHERIES LIMITED * P. O. Box 546 * GEITA

MBELE YA
JINA. Kevin K. Rweikiza.....
SAINI.....
WADHIFA. Mwanasheria.....

COUNCIL SOLICITOR :: UKEREWE DISTRICT COUNCIL :: P.O. BOX 41 NANSIO UKEREWE